JAMES KALEKWA



# MIMI NI MWANAMUME

# MIMI

# NI

# MWANAMUME.

James Kalekwa

## Orodha ya Yaliyomo

Utangulizi ........................................ 4
Msuli #1. Wa kiume (Male) ........................................ 4
Msuli #2. Mwanamume (Man) ........................................ 7
Msuli #3: MUME ........................................ 11
Msuli #4. BABA ........................................ 13
Kuhusu Mwandishi: ........................................ 16
Kuhusu New Vine Church: ........................................ 17
Mawasiliano na Mwandishi: ........................................ 17

## Utangulizi

Nina utafsiri uanaume kwa madaraja makubwa manne ambayo ninayaita misuli. Kila mwanamume ana mahali fulani ambapo huchota tafsiri yake ya uanaume. Na tafsiri hiyo ndiyo huamua kila kitu kuhusian na yeye kwenye maisha.

Nimekikusudia kitabu kuchochea ufikiri ndani yako mwanamume mwenzangu badala ya kukupa risala tu.

Utagundua unaposoma ni kama umeingia “gym”, mkufunzi hukuanzishia zoezi fulani kisha wewe ndiye unapaswa kuendelea kwenye hilo zoezi ili upate matokeo. Ndicho ninachofanya kwenye kitabu hiki.

Karibu tujenge misuli mine ya uanaume!

## Msuli #1. Wa kiume (Male)

Umewahi kuona wazazi ambao wanasubiri kwa shauku kupokea mzaliwa wao wa kwanza? Mama mjamzito yuko chumba cha kujifungulia (labour ward). Huku nje wengine wote wana maswali mengi sana. Na mojawapo ya swali ni motto wa jinsia gani amekuja. Kimsingi, baada ya zoezi la kujifungua kwenda salama, muuguzi au mkunga huja na neno “hongera sana” kisha kinachofuata huwa ni kumtambulisha mtoto ni wa jinsia gani.

Unadhani kigezo gani hutumika kuamua ya kwamba huyu ni mtoto wa kike ua mtoto wa kiume?

Ni maumbile yake; ni viungo vyake vya uzazi.

Na hii ndiyo tafsiri ya kwanza na ya awali ya uanaume ambayo mtu huipata.  Hii ni ya kuzaliwa. Ni zawadi kutoka kwa Mungu. Ni tafsiri unayopewa kutokea kwenye maumbile yako.

Kuna sehemu ambayo tabibu, muuguzi, mkunga hutazama na kisha hutoa habari njema kwa mama mzazi "Hongera umepata mtoto wa kiume". Hiyo sehemu inaitwa UUME!

Huhitaji kufanya chochote, huhitaji bidii yoyote kuwa wa kiume (male).

**Upande Mzuri:**
Ni vyema kuanzia hapo kupata tafsiri ya uanaume wako. Dunia tunayoishi sasa hivi, kuna hali ya kuchanganyikiwa kwingi sana. Yaani, kuna watu wa kiume lakini hawana uhakika au ujasiri na kiashiria cha maumbile yao.

Uwepo wa maumbile yako ya kiume ukupe tafsiri ya kwamba, Mungu amekupa zawadi ya kuwa mwanadamu mwanamume.

**Upande Mbaya:**
Hata hivyo tafsiri ya uanaume wako hawapaswi kugotea kwenye maumbile tu. Unapaswa kwenda zaidi ya maumbile yako.

Wale ambao hubakia kwenye maumbile, ndiyo huenda mbali zaidi na kujivunia misuli, kifua, mwonekano wa nje; na kwa upande mwingine, kuna

wale hujiona ni duni au wanaume pungufu kwa sababu ya kutokuwa na umbile fulani – mwonekano fulani wa kimwili. Kwa sababu wao wamegotea uanaume wao kwenye maumbile!

Hatari za wa kubakiza tafsiri ya uanamume kwenye maumbile ni kuishi kuwa mharibifu (violent) - unaweza kubaka, kupiga ngumi, kutukana, kutishia kwa sababu wewe ni mwanamume (yaani una maumbile fulani)

**Unafahamu kisa cha AMNONI?**

*11 Naye alipokwisha kuileta karibu naye, ili ale, Amnoni akamkamata, akamwambia, Njoo ulale nami, ndugu yangu.*

*12 Naye akamjibu, La, sivyo, ndugu yangu, usinitenze nguvu; kwani haifai kutendeka hivi katika Israeli; usitende upumbavu huu.*

2 Samweli 13:11-12

**Kwanini alifanya hivyo?**

Sababu ya NGUVU – tafsiri ya uanaume kutokea kwenye maumbile ya kimwili tu. Alijitafsiri kuwa mwanamume kwa nguvu alizokuwa nazo.

Umewahi kusikia nyimbo, tungo, machapisho au vyombo vya habari vikimuwasilisha mwanamume kwa tafsiri ya maumbile ya kimwili tu?

Mwanamume yeyote anayejipatia tafsiri ya uanaume wake kwa njia hii tu, anabaki kuwa kwenye hali ya utoto. Kwa sababu watoto wanapewa tafsiri ya uanaume na maumbile yao.

Hebu jiulize hivi, mtoto hutofautishaje ya kwamba huyu ni wa kiume na huyu ni wa kike? Kwa kutazama maumbile tu. Mwonekano wa kimwili.

## Msuli #2. Mwanamume (Man)

*"Mimi naenda njia ya ulimwengu wote; basi uwe hodari, ujionyeshe kuwa mwanamume;"*
**1 Wafalme 2:2**

Ukiambiwa ujionyeshe kuwa mwanamume, utaonyesha nini?

Jambo la uhakika najua hutaonyesha ni maumbile yako. Huwezi kutembea umefungua zipu ili watu watambue wewe ni mwanamume. Jambo la uhakika hutaonyesha maungo au maumbile yako.

Kama ni kweli, utaonyesha nini sasa kaka?

Ni kweli. Hatua ya kuwa mwanamume ni zaidi ya maungo/maumbile.

Hapa, mwanamume hujipatia tafsiri ya yeye ni nani kutokea kwenye mkusanyiko wa uelewa, fikra, mitazamo, mafunzo... ni NAFSI! Ni utu wa ndani!

Ukisoma kwa umakini andiko hilo utaona kabisa uanaume ni kuonyesha utu wa ndani ulioathiriwa na roho yako!

*"shika lile Bwana Mwenyezi Mungu wako analokuagiza: Enenda katika njia zake, ushike maagizo na amri zake, sheria zake na kanuni zake, kama ilivyoandikwa katika Torati ya Musa, ili upate kustawi katika yote ufanyayo na popote uendako,"*
**1 Wafalme 2:3 NMM**

Unaona kujionyesha kuwa mwanamume kunaanzia wapi?

Mahusiano binafsi na Mungu. Mkazo wangu uko kwenye mahusiano BINAFSI.

Kwa mwanamume, kuokoka, ndiyo habari ya kwanza na ya muhimu! Ndiyo kiwango cha juu sana cha kujitambua. Kutokuokoka ni kiwango cha juu sana cha kiburi.

Mwanamume ambaye hana mahusiano binafsi na Mungu ni bomu linalosubiria muda wa kulipuka... ni hatari sana!

Hata hivyo, nikupeleke mbele kidogo; kwenye huo mstari wa 3 kuna vitu vinaorodheshwa hapo:

1. Njia
2. Maagizo
3. Amri
4. Sheria
5. Kanuni

Kaka, hayo mambo ni makubwa mno asee!!!
Haya ndiyo yanamtengeneza mwanamume.

Daudi anamwonyesha mwanae namna ya kuwa mwanamume.

- Mwanamume ni mtu anayemwabudu Mungu kwa kujimwaga bila kujali maoni ya watu. Unamkumbuka Daudi alivyojiachia mbele za Bwana machoni pa mke wake (Mikali binti Sauli)? Hebu soma maelezo ya ibada ya sifa:

*"Ndipo Daudi akarudi ili awabarikie watu wa nyumbani mwake. Na Mikali, binti Sauli, akatoka nje aende kumlaki Daudi, naye akasema, Mfalme wa Israeli alikuwa mtukufu leo namna gani, akijifunua mwili wake mbele ya vijakazi vya watumishi wake,*

*mfano wa watu baradhuli mmojawapo, ajifunuavyo mwili wake mbele ya watu, asipokuwa na haya!"*

**2 Samweli 6:20**

Anajifunua kama baradhuli (kichaa/mtu aliyerukwa na akili/mtu asiye mstaarabu)

Yaani, aliabudu mpaka akaoneka hivyo.

Halafu sikia MAJIBU ya mwanamume:

*"21 Daudi akamwambia Mikali, Ilikuwa mbele za Bwana, aliyenichagua mimi juu ya baba yako, na juu ya nyumba yake, ili kuniweka niwe mkuu juu ya watu wa Bwana, juu ya Israeli; kwa hiyo mimi nitacheza mbele za Bwana."*
*22 Kisha nitakuwa hafifu zaidi, nami nitakuwa mnyonge machoni pangu mimi mwenyewe; lakini kwa wale vijakazi uliowanena, kwao nitaheshimiwa."*
**2 Samweli 6:21-22**

- Mwanamume ni kuishi zaidi yako... kuishi kwa ajili ya jambo kubwa kuliko wewe. Tena, ni kuwawazia wengine (mindful) juu ya namna unavyoishi.

Mwanamume hutumia nguvu zake nyingi kuwalinda wanyonge, duni, wasiojiweza na wanaoonewa!

Na hii ndiyo sababu kwanini wanaume wa Biblia ndiyo walikuwa wakienda vitani na kuacha wanawake na watoto wadogo nyumbani. Kutumia nguvu zao kwa ajili ya watu wao.

Nguvu uliyopewa si kwa ajili ya kuwadhuru watu wako bali kuwalinda.

- Mwanamume, hujali (considerate) hisia za watu wengine; hawagandamizi au kuwatumia tu ili kukidhi hamu au nataka yake. Mwanamume afanyaye hivyo huleta madhara makubwa sana.

Unakumbuka madhara ya tukio moja la kaka Amnoni? Familia ya mfalme Daudi ilinajisika kwa shina la uchungu [Soma kitabu nilichoandika cha **Shujaa Aliyejeruhiwa**]

## Msuli #3: MUME

Hii ni ngazi kubwa sana ya kimahusiano hapa duniani. Yaani, kuamua kwa hiyari yako mwenyewe...

"Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja."
Mwanzo 2:24

Kukubali kuhusiana na mtu mmoja kwa kiwango kikubwa cha kimahusiano kuliko mtu mwingine yeyote. Kuyashiriki maisha yako na mtu mwingine.

Si kwamba hakuna wanawake wazuri. Tena inawezekana kumzidi huyo mwanamke ambaye atakuwa mke wako... wanazaliwa wazuri zaidi. Hata hivyo, mwanamume wa ngazi hii (mume) hufanya maamuzi na kusimama nayo!

Si ajabu Biblia inatufunulia ya kwamba...

*"Mtu aziniye na mwanamke hana akili kabisa; Afanya jambo litakalomwangamiza nafsi yake."*
**Mithali 6:32**

Hebu nikutazamishe tena kina kingine cha mwanamume wa ngazi hii (mume). Kwa kifupi tu, kuwa MUME ni kupewa fursa ya kuonyesha nafasi ya Kristo kwa kanisa... kwa mke wako!

Iko hivi,

Kristo ndiye Bwana arusi; ndiye mume wa kanisa. Na mke wako ni sehemu ya hilo kanisa.

Sasa ukioa, unaagizwa hivi:

*“25 Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake;*

*28 Vivyo hivyo imewapasa waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe. Ampendaye mkewe hujipenda mwenyewe."*

**Waefeso 5:25, 28**

Kipimo cha upendo ni Kristo kwa kanisa. Kwa hiyo, kama mke wako anataka kujua upendo wa Kristo... anapaswa kukuangalia wewe! Ana mahala pa kujifunza. Yaani, mume... yaani wewe!

Huoni kuwa mume ni *"hatari"* sana?

Kuwa mume ni kupokea jukumu la kumfunua Kristo kwa mke wako... ndiyo maana unapaswa kulipokea hili jukumu kwa unyenyekevu sana na kutetemeka. Hebu fikiria jinsi ambavyo wavulana (watu wanaojipatia tasfiri ya uanaume kwa njia ya maungo na maumbile tu) wanamuabisha sana Yesu huko kwenye ndoa. Yaani, ni watu wambao kitu pekee wanaweza kutoa ni maungo na maumbile yao tu. Mke hawezi kumuona Kristo kwa mume mvulana!

## Msuli #4. BABA

Si unafahamu Mungu hujitambulisha kama BABA yetu aliye mbinguni (Mathayo 6:9) ... au BABA wa yatima (Zaburi 68:5)?

Baba ni chanzo... kupitia wewe kuna watu watakuja duniani. Watakuwa na vinasaba vyako, kundi la damu lako, jina lako.

Kuwa baba ni kukubali majukumu kama ya BABA yetu wa mbinguni... si unajua tukimaliza kumsifia huwa tunamwambia *"utupe leo mkate wetu wa kila siku..."?*

Ni majukumu!

Si unajua tukimwomba mkate hatupi jiwe? Na hatupi nyoka kama majibu ya samaki?

Ni MAJUKUMU!

Kuwa baba ni kukubali kuishi kwa ajili ya watu wengine na vizazi vingi vinavyokuja. Katika yote unayoyatenda unapaswa kuwawazia wengine.

Upokee huu ukweli ya kwamba kuwa baba ni zaidi ya kuweza kutungisha mimba.

Mojawapo ya mambo ambayo unapaswa kuyarithisha kwa uzao wako:

- Kumrithisha Mungu kwa vizazi vyako
- Kurithisha jina (hapa sina maana ya ubini; bali heshima inayoambatana na jina)
- Kurithisha mali na fedha
- Kurithisha mifumo
- Kuwa baba ni kuandaa vitu na watu kwa ajili ya kizazi kianachofuata (1 Nyakati 22:1-7)

Kwenye kitabu hiki nimekusudia kuanza kukufikirisha kuhusu dhana ya ubaba zaidi ya watoto wako wa kibaiolojia au wa jamaa zako.

Kuna ubaba ambao ni kupewa heshima kwenye mioyo ya watu kama kiongozi, kielelezo na mtu mwenye mamlaka. Ni kuwa *"father figure".*

Kwa sababu za kuenea kwa dhambi na uovu na sababu zingine, kuna watu kwenye jamii hawatakuwa na baba zao au watakuwa na baba watoro (passive fathers). Hii ndiyo sababu wanahitajika akina baba wa muundo huu.

Mwanamume unapaswa kuweka lengo la kuishi kwa namna ambayo utafikia daraja la kuwa "father figure" kwa wengine. Unapaswa kuwaza zaidi ya watoto wako. Iwaze jamii; Iwaje nchi; kiwaze kizazi chetu na vizazi vinavyofuata.

**Muunganiko wa ubaba na BABA:**

Namna unavyohusiana na watoto (watu waliochini ya ubaba wako, wa kibaioojia au ubaba wa heshima) inapaswa iwaelekeze kuhusu ubaba na hatimaye wamfahamu BABA wa mbinguni. Ni kuwa uakisi (reflection) wa BABA wa mbinguni. Kuwa baba ni kuaminiwa na Mungu kumfunua anafananaje.

Jambo hili ni la kuchukua kwa heshima sana.

Na hicho ndiyo kiwango kikubwa cha uanaume!

## Kuhusu Mwandishi:

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

## Kuhusu New Vine Church:

Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: [https://www.newvinechurch.or.tz](https://www.newvinechurch.or.tz)

## Mawasiliano na Mwandishi:

Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi n audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: [https://t.me/nvcdodoma](https://t.me/nvcdodoma) AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: James Kalekwa

Instagram: james_kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia +255-754-917-7764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

# KUHUSU MWANDISHI



**James Kalekwa** ni amemwamini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa Maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis “Tai”, Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma.


James Kalekwa

james_kalekwa

@MchungajiJK

+255 754 917 764